

JUMAPILI YA MATAWI



SHAIRI LA SIKU

Hosana kwa Mwana wa Daudi! Mubarikiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosana juu mbinguni!

Matayo 21:9

Injili ya kuingia Yerusalema inaweza kusomwa mwanzoni mwa ibada mbele kutembea na matawi.

HABARI NJEMA

Luka 19:29-40

Sikieni Habari Njema takatifu kama lilivyoandikwa katika Injili ya Luka Mtakatifu.

Utukufu uwe nawe, Ee Bwana wetu.

Ikawa alipokaribia Bethfage na Bethania, kwenye mlima uitwao wa Mizeituni, alituma wawili katika wale wanafunzi, akisema, Nendeni mpaka katika kijiji kile kinachowakabili, na mtakapoingia ndani mtaona mwanapunda, amefungwa, ambaye hajapandwa na mtu yeyote bado, mfungueni mkamlete hapa. Na kama mtu akiwauliza, Mbona mnamfungua? Semeni hivi, Bwana anamhitaji. Na wale waliotumwa wakaenda wakaona kama alivyowaambia. Na walipokuwa wakimfungua mwanapunda, wenyewe waliwaambia, Mbona mnamfungua mwanapunda? Wakasema, Bwana anamhitaji. Wakampeleka kwa Yesu, wakatandika nguo zao juu ya mwanapunda, wakampandisha Yesu. Na alipokuwa akienda walitandaza nguo zao njiani. Na alipokuwa amekaribia mteremko wa mlima wa Mizeituni, kundi zima la wanafunzi wake walianza kufurahi na kumsifu Mungu kwa sauti kuu, kwa ajili ya matendo yote ya uwezo waliyoyaona, wakasema, Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana; amani mbinguni, na utukufu huko juu. Baadhi ya Mafarisayo walio-kuwa katika mkutano wakamwambia, Mwalimu, uwakanye wanafunzi wako. Akajibu, akasema, Nawaambia ninyi, wakinyamaza hawa, mawe yatanena kwa sauti kuu.

Mwisho wa kusoma Habari Njema, musomaji aseme:

Hii ndiyo Habari Njema ya Kristo.

Tunakusifu sana, Ee Kristo, kwa Habari Njema yako takatifu.

WIMBO WA KUINGILIA

Wote kusimama

WITO WA KUABUDU

Tumekusanyika pamoja kama jamaa ya Mungu mbele ya Baba yetu, tukivutwa na Roho yake, kusifu Jina lake, kusikia na kupokea Neno lake takatifu. kumwomba usamehe kwa zambi zetu, kuomba mahitaji yetu na ya dunia, kufurahi katika mapendo yake, na kutumwa katika salama yake.

MWALIKO

Ee Bwana, ufungue midomo yetu.

Na kinywa chetu kitaonyesha sifa yako.

Katika KUJA na KUFUNGA:

Tumaini letu ni katika jina la Bwana.

Aliyeumba mbingu na dunia.

Ee Mungu, utuokoe kwa haraka.

Ee Bwana wetu, utusaidie kwa haraka.

Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine.

WIMBO

OPENING SENTENCE

Hosanna to the Son of David! Blessed is he who comes in the name of the Lord! Hosanna in heaven!

Matthew 21:9

The Gospel of entering Jerusalem can be read at the beginning of the service before walking with the branches.

THE GOSPEL READING

Luke 19:29-40

Hear the holy Gospel, as it is written in the Gospel of St. Luke.

Glory be to you, O Lord.

When he had come near Bethphage and Bethany, at the place called the Mount of Olives, he sent two of the disciples, saying, 'Go into the village ahead of you, and as you enter it you will find tied there a colt that has never been ridden. Untie it and bring it here. If anyone asks you, "Why are you untying it?" just say this: "The Lord needs it."' So those who were sent departed and found it as he had told them. As they were untying the colt, its owners asked them, 'Why are you untying the colt?' They said, 'The Lord needs it.' Then they brought it to Jesus; and after throwing their cloaks on the colt, they set Jesus on it. As he rode along, people kept spreading their cloaks on the road. As he was now approaching the path down from the Mount of Olives, the whole multitude of the disciples began to praise God joyfully with a loud voice for all the deeds of power that they had seen, saying, 'Blessed is the king who comes in the name of the Lord! Peace in heaven, and glory in the highest heaven!' Some of the Pharisees in the crowd said to him, 'Teacher, order your disciples to stop.' He answered, 'I tell you, if these were silent, the stones would shout out.'

After reading the Gospel, the reader says:

This is the Gospel of Christ.

Praise be to you, O Christ, for your holy Gospel.

PROCESSIONAL HYMN

Stand for the Procession

CALL TO WORSHIP

We are gathered together as God's family before our Father, drawn by his Spirit, to praise his Name, to hear and receive his holy Word. to ask him to forgive us for our sins, to pray for our needs and the needs of the world, to rejoice in his love, and to be sent to his safety.

INVITATORY

O Lord, open our lips.

And our mouth shall proclaim your praise.

At ADVENT and LENT:

Our hope is in the name of the Lord.

Who created heaven and earth.

O God, make speed to save us.

O our Lord, make haste to help us.

A song from the Bible or another song is sung.

HYMN

Muhudumu aseme:

Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu. Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atatuondolea zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.

I Yoane 1:8-9

Muhudumu aseme:

Tukiri zambi zetu kwa Mungu Mwenyezi.

Wote wapige magoti na kusema

Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, tumekosea wewe, na tumekosea jirani zetu, kwa mawazo yetu, na kwa maneno yetu, na kwa matendo yetu, na kwa maovu tuliyoyatenda, na kwa mema tusiyoyatenda, kosa letu wenyewe. Sisi tunatubu kabisa. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote yaliyopita; utuwezeshe tangu leo kukutumikia, katika upya wa uzima. Kwa utukufu wa Jina lako. Amina.

Muhudumu au mutu mwengine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.

Ee Mungu, mwenye rehema, tunakusihhi, utupe sisi, watu wako waaminifu, usamehe na salama, ili tusafishwe zambi zetu zote, na tukutumikie na nia tulivu; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Wote **Amina.**

Zaburi ya Siku isomwe au iimbwe. Watu wote walisoma nusu ya mstari baada ya msomaji.

ZABURI 31:9-36

9 Ee BWANA, unifadhili, maana ni katika dhiki, Jicho langu limenyauka kwa masumbufu, **Naam, mwili wangu na nafsi yangu.**

10 Maana maisha yangu yamekwisha kwa huzuni, Na miaka yangu kwa maumivu. **Nguvu zangu zimeniishia kwa uovu wangu, Na mifupa yangu imepooza.**

11 Kwa sababu ya watesi wangu nimelaumiwa, Naam, hasa kwa jirani zangu; **Na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu; Wanaoniona njiani wananikimbia.**

12 Nimesahauliwa kama mfu asiyekumbukwa;

Nimekuwa kama chombo kilichovunjika.

13 Maana nimesikia wengi wakinong'onezana; Hofu katika pande zote.

Waliposhauriana juu yangu, Walipanga kunitoa uhai wangu.

14 Lakini mimi nakutumaini Wewe, BWANA,

Nimesema, Wewe ndiwe Mungu wangu.

15 Nyakati zangu zimo mikononi mwako;

Uniponye kutoka kwa adui zangu na wanaonifuatia.

16 Umwangaze mtumishi wako Kwa nuru ya uso wako;

Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:

kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa, hata milele na milele. Amina.

CONFESSION OF SIN

The Minister should say:

If we say that we have no sin, we deceive ourselves, and the truth is not in us. If we confess our sins, he who is faithful and just will forgive us our sins and cleanse us from all unrighteousness.

1 John 1:8-9

The Minister should say:

Let us confess our sins to God Almighty.

All should kneel and say:

Almighty God, our heavenly Father, we have sinned against you and against our neighbors, in thought and word and deed, in the evil we have done and in the good we have not done, through our own deliberate fault. We are truly sorry, and repent of all our sins. For the sake of your Son Jesus Christ, who died for us, forgive us all that is past; and grant that we may serve you in newness of life to the glory of your name. Amen.

A minister or other person who is not a priest, kneeling should use this request:

Grant, we ask you, merciful Lord, to your faithful people pardon and peace, that they may be cleansed from all their sins, and serve you with a quiet mind, through Jesus Christ our Lord.

All Amen.

The Psalm of the Day should be read or sung. All the people read half a line after the reader.

PSALM 31:9-36

9 Be gracious to me, O Lord, for I am in distress; my eye wastes away from grief,
my soul and body also.

10 For my life is spent with sorrow and my years with sighing;
my strength fails because of my misery, and my bones waste away.

11 I am the scorn of all my adversaries, a horror to my neighbors,
an object of dread to my acquaintances; those who see me in the street flee from me.

12 I have passed out of mind like one who is dead;
I have become like a broken vessel.

13 For I hear the whispering of many— terror all around!—
as they scheme together against me, as they plot to take my life.

14 But I trust in you, O Lord;
I say, “You are my God.”

15 My times are in your hand;
deliver me from the hand of my enemies and persecutors.

16 Let your face shine upon your servant;
save me in your steadfast love.

Glory be to the Father, and to the Son, and to the Holy Spirit:

As it was in the beginning, is now, and ever shall be, world without end. Amen.

HYMN

AGANO LA KALE

Isaya 50:4-9a

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Kitabu cha Isaya.

Bwana MUNGU amenipa ulimi wa hao wafundishwao, nipate kujua jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka, huniamsha asubuhi baada ya asubuhi; huniamsha, sikio langu lipate kusikia kama watu wafundishwao. Bwana MUNGU amenizibua sikio langu, wala sikuwa mkaidi, wala sikurudi nyuma. Niliwatolea wapigao mgongo wangu, na wang'oao ndevu mashavu yangu; sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate. Maana Bwana MUNGU atanisaidia; kwa sababu hiyo sikutahayari, kwa sababu hiyo nimekaza uso wangu kama jiwe, nami najua ya kuwa sitaona haya. Yeye anipatiaye haki yangu yu karibu; ni nani atakayeshindana nami? Na tusimame pamoja; ni nani aliye hasimu yangu? Na anikaribie basi. Tazama, Bwana MUNGU atanisaidia; ni nani atakayenihukumu kuwa mwenye hatia?

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO

Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO JIPIYA kisomwe.

AGANO JIPIYA

Wafilipi 2:5-11

Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Barua ya Paulo Mtume kwa Wafilipi.

Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuko na namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO

MATESO YA BWANA WETU YESU KRISTO KULINGANA NA LUKA MTAKATIFU

HABARI NJEMA

Luka 23:1-49

Watu wote wanapaswa kuketi chini kwa ajili ya kuanza kusoma Injili

Kisha mkutano wote wakasimama, wakampeleka kwa Pilato. Wakaanza kumshitaki, wakisema, Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme. Pilato akamwuliza, akisema, Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Akajibu akamwambia, Wewe wasema. Pilato akawaambia wakuu wa makuhani na mkutano, Sioni neno lililo ovu katika mtu huyu. Nao walisisitiza sana, wakisema, Huwataharakisha watu, akifundisha katika Yudea yote, tokea Galilaya mpaka huku. Pilato aliposikia hayo aliuliza kama huyu ni mtu wa Galilaya. Na alipopata habari ya kuwa yu chini ya mamlaka ya Herode, alimpeleka kwa Herode, kwa kuwa yeye naye alikuwapo Yerusalemu siku zile. Herode alipomwona Yesu alifurahi sana, kwa sababu alikuwa akitaka sana kumwona

All Sit. A passage from the OLD TESTAMENT should be read.

FIRST READING

Isaiah 50:4-9a

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Book of Isaiah.

The Lord God has given me the tongue of a teacher, that I may know how to sustain the weary with a word. Morning by morning he wakens-- wakens my ear to listen as those who are taught. The Lord God has opened my ear, and I was not rebellious, I did not turn backward. I gave my back to those who struck me, and my cheeks to those who pulled out the beard; I did not hide my face from insult and spitting. The Lord God helps me; therefore I have not been disgraced; therefore I have set my face like flint, and I know that I shall not be put to shame; he who vindicates me is near. Who will contend with me? Let us stand up together. Who are my adversaries? Let them confront me. It is the Lord God who helps me; who will declare me guilty?

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

All Sit. A passage from the NEW TESTAMENT should be read.

SECOND READING

Philippians 2:5-11

Let the reader say first:

Hear the Word of the Lord as written in the Letter of the Apostle Paul to the Philippians.

Let the same mind be in you that was in Christ Jesus, who, though he was in the form of God, did not regard equality with God as something to be exploited, but emptied himself, taking the form of a slave, being born in human likeness. And being found in human form, he humbled himself and became obedient to the point of death-- even death on a cross. Therefore God also highly exalted him and gave him the name that is above every name, so that at the name of Jesus every knee should bend, in heaven and on earth and under the earth, and every tongue should confess that Jesus Christ is Lord, to the glory of God the Father.

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

THE PASSION OF OUR LORD JESUS CHRIST ACCORDING TO SAINT LUKE

GOSPEL READING

Luke 23:1-49

All people should sit for the beginning of reading the Gospel

Then the assembly rose as a body and brought Jesus before Pilate. They began to accuse him, saying, 'We found this man perverting our nation, forbidding us to pay taxes to the emperor, and saying that he himself is the Messiah, a king.' Then Pilate asked him, 'Are you the king of the Jews?' He answered, 'You say so.' Then Pilate said to the chief priests and the crowds, 'I find no basis for an accusation against this man.' But they were insistent and said, 'He stirs up the people by teaching throughout all Judea, from Galilee where he began even to this place.' When Pilate heard this, he asked whether the man was a Galilean. And when he learned that he was under Herod's jurisdiction, he sent him off to Herod, who was himself in Jerusalem at that time. When Herod saw Jesus, he was very glad, for he had been wanting to see him for a long time,

tangu siku nyingi, maana amesikia habari zake, akatarajia kuona ishara iliyofanywa na yeye. Akamwuliza maneno mengi, yeye asimjibu lolote. Wakuu wa makuhani na waandishi wakasimama wakamshitaki kwa nguvu sana. Basi Herode akamdhalilisha, pamoja na askari wake, akamdhihaki, na kumvika mavazi mazuri; kisha akamrudisha kwa Pilato. Basi siku ile ile Herode na Pilato walipatana kwa urafiki kwa maana hapo kwanza walikuwa na uadui wao kwa wao. Na Pilato akawakutanisha wakuu wa makuhani, na wakubwa, na watu, akawaambia, Mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotosha watu; nami, tazama, nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lolote katika mambo hayo mliyomshitaki; wala hata Herode, kwa maana amemrudisha kwetu; basi tazama, hakuna neno lolote alilolitenda lipasalo kufa. Kwa hiyo nitamrudi, kisha nitamfungua. [Maana ilimlazimu kuwafungulia mfungwa mmoja wakati wa sikukuu.] Wakapiga kelele wote pamoja, wakisema, Mwondoe huyu, utufungulie Baraba. Naye ni mtu aliyetupwa gerezani kwa ajili ya fitina iliyotokea mjini, na kwa uuaji Basi Pilato alisema nao mara ya pili, kwa vile alivyotaka kumfungua Yesu. Lakini wakapiga kelele, wakisema, Msulubishe. Msulubishe. Akawaambia mara ya tatu, Kwa sababu gani? Huyu ametenda uovu gani? Sikuona kwake hata neno lipasalo kufa. Basi nikiisha kumrudi nitamfungua. Lakini wakatoa sauti zao kwa nguvu sana, wakitaka asulubiwe. Sauti zao zikashinda. Pilato akahukumu kwamba haja yao ifanyike. Akamfungua yule aliyetupwa gerezani kwa ajili ya fitina na uuaji, yule waliyemtaka, akamtoa Yesu wamfanyie watakavyo. Na walipokuwa wakimwondoa walimkamata mtu mmoja, Simoni Mkirene, aliyekuwa ametoka shambani, wakamtwika msalaba, auchukue nyuma yake Yesu. Mkutano mkubwa wa watu wakamfuata, na wanawake waliokuwa wakijipiga vifua na kumwombolezea. Yesu akawageukia, akasema, Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi, bali jililieni nafsi zenu na watoto wenu. Kwa maana tazama, siku zitakuja watakaposema, Heri walio tasa, na matumbo yasiyozaa, na maziwa yasiyonyonyesha. Ndipo watakapoanza kuiambia milima, Tuangukieni, na vilima, Tufunikeni. Kwa kuwa kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, itakuwaje katika mkavu? Wakapelekwa na wawili wengine, wahalifu, wauawe pamoja naye.

Watu wote wasimame

Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulubisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kulia, na mmoja upande wa kushoto. Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake, wakipiga kura. Watu wakasimama wakitazama. Wale wakuu nao walikuwa wakimfanyia mzaha, wakisema, Aliokoa wengine; na ajiokoe mwenyewe, kama ndiye Kristo wa Mungu, mteule wake. Wale askari nao wakamfanyia dhahaka, wakimwendea na kumletea siki, huku wakisema, Kama wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi, ujiokoe mwenyewe. Na juu yake palikuwa na anwani; HUYU NDIYE MFALME WA WAYAHUDI. Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akisema, Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu akamkemea, akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lolote lisilofaa. Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi. Hapo ilikuwa yapata saa sita, kukawa giza juu ya nchi yote hadi saa tisa, jua limepungua nuru yake; pazia la hekalu likapasuka katikati. Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu. Alipokwisha kusema hayo alikata roho. Yule jemadari alipoona yaliyotukia, alimtukuza Mungu, akisema, Hakika yake, mtu huyu alikuwa mwenye haki. Na makutano yote ya watu waliokuwa wamekutanika kutazama mambo hayo, walipoona yaliyotendeka, wakaenda zao kwao, wakijipigapiga vifua. Na wote waliojuana naye, na wale wanawake walioandamana naye toka Galilaya, wakasimama kwa mbali, wakitazama mambo hayo.

Hilo ndilo Neno la Bwana.
Asante kwa Mungu.

because he had heard about him and was hoping to see him perform some sign. He questioned him at some length, but Jesus gave him no answer. The chief priests and the scribes stood by, vehemently accusing him. Even Herod with his soldiers treated him with contempt and mocked him; then he put an elegant robe on him, and sent him back to Pilate. That same day Herod and Pilate became friends with each other; before this they had been enemies. Pilate then called together the chief priests, the leaders, and the people, and said to them, 'You brought me this man as one who was perverting the people; and here I have examined him in your presence and have not found this man guilty of any of your charges against him. Neither has Herod, for he sent him back to us. Indeed, he has done nothing to deserve death. I will therefore have him flogged and release him.' Then they all shouted out together, 'Away with this fellow! Release Barabbas for us!' (This was a man who had been put in prison for an insurrection that had taken place in the city, and for murder.) Pilate, wanting to release Jesus, addressed them again; but they kept shouting, 'Crucify, crucify him!' A third time he said to them, 'Why, what evil has he done? I have found in him no ground for the sentence of death; I will therefore have him flogged and then release him.' But they kept urgently demanding with loud shouts that he should be crucified; and their voices prevailed. So Pilate gave his verdict that their demand should be granted. He released the man they asked for, the one who had been put in prison for insurrection and murder, and he handed Jesus over as they wished. As they led him away, they seized a man, Simon of Cyrene, who was coming from the country, and they laid the cross on him, and made him carry it behind Jesus. A great number of the people followed him, and among them were women who were beating their breasts and wailing for him. But Jesus turned to them and said, 'Daughters of Jerusalem, do not weep for me, but weep for yourselves and for your children. For the days are surely coming when they will say, "Blessed are the barren, and the wombs that never bore, and the breasts that never nursed." Then they will begin to say to the mountains, "Fall on us"; and to the hills, "Cover us." For if they do this when the wood is green, what will happen when it is dry?' Two others also, who were criminals, were led away to be put to death with him.

The People Stand

When they came to the place that is called The Skull, they crucified Jesus there with the criminals, one on his right and one on his left. [Then Jesus said, 'Father, forgive them; for they do not know what they are doing.'] And they cast lots to divide his clothing. And the people stood by, watching; but the leaders scoffed at him, saying, 'He saved others; let him save himself if he is the Messiah of God, his chosen one!' The soldiers also mocked him, coming up and offering him sour wine, and saying, 'If you are the King of the Jews, save yourself!' There was also an inscription over him, 'This is the King of the Jews.' One of the criminals who were hanged there kept deriding him and saying, 'Are you not the Messiah? Save yourself and us!' But the other rebuked him, saying, 'Do you not fear God, since you are under the same sentence of condemnation? And we indeed have been condemned justly, for we are getting what we deserve for our deeds, but this man has done nothing wrong.' Then he said, 'Jesus, remember me when you come into your kingdom.' He replied, 'Truly I tell you, today you will be with me in Paradise.' It was now about noon, and darkness came over the whole land until three in the afternoon, while the sun's light failed; and the curtain of the temple was torn in two. Then Jesus, crying with a loud voice, said, 'Father, into your hands I commend my spirit.' Having said this, he breathed his last. When the centurion saw what had taken place, he praised God and said, 'Certainly this man was innocent.' And when all the crowds who had gathered there for this spectacle saw what had taken place, they returned home, beating their breasts. But all his acquaintances, including the women who had followed him from Galilee, stood at a distance, watching these things.

The Word of the Lord.

Thanks be to God.

WIMBO WA INJILI

KUHUBIRI

Bikole Mulanda, *Waziri wa Usharika wa Kiswahili*

IMANI YA MITUME

Watu wasimame kuhakikisha IMANI YA MITUME

Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia; Na Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu, aliyetwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu, akazaliwa na Bikira Maria. Akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimuni mwa wafu, akafufuka katika wafu siku ya tatu, akapanda mbinguni, anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu, Baba Mwenyezi, ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu. Ninamwamini Roho Mutakatifu, Kanisa katolika takatifu, ushirika wa watakatifu, on-doleo la zambi, ufufuko wa mwili, na uzima wa milele. Amina.

MAOMBI

Kupiga magoti

Muhudumu Bwana utuhurumie.

Wote **Kristo utuhurumie.**

Muhudumu Bwana utuhurumie.

SALA YA BWANA

Wote

Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku; utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe waliotukosea. Usitulete katika majaribu, lakini utuokoe katika uovu. Kwani kwako ufalme, uwezo na utukufu, milele na milele, Amina.

Muhudumu Ee Bwana utuonyeshe rehema yako;

Wote **Utupe sisi wokovu wako.**

Muhudumu Ee Bwana uwabariki watawala wetu;

Wote **Utusikie kwa rehema yako tukikuomba.**

Muhudumu Uwavike haki wahudumu wako;

Wote **Uwafurahishe wachaguliwa wako.**

Muhudumu Ee Bwana uwaokoe watu wako;

Wote **Uubariki uriti wako.**

Muhudumu Ee Bwana utupe salama kwa siku zetu;

Wote **Na utukufu wako uwe popote duniani.**

Muhudumu Ee Mungu, utusafishe mioyo yetu;

Wote **Na ututegemeze na Roho yako Mutakatifu.**

SALA YA SIKU

Mungu Mweyezi wa milele, kwa mapendo yako makuu kwa watu wote, ulimutuma Mwana wako, Mwokozi wetu, Yesu Kristo, kutwaa mwili wetu, na kuvumilia mauti ya musalaba, utupe sisi, kufuata mufano wa uvumilivu na unyenyekevu zake, na vile kushiriki katika kufufuka kwake, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

HYMN OF THE GOSPEL

SERMON

Bikole Mulanda, *Swahili Minister*

THE APOSTLES' CREED

All People should stand and say the APOSTLES' CREED:

I believe in God, the Father almighty, creator of heaven and earth; I believe in Jesus Christ, his only Son, our Lord. He was conceived by the power of the Holy Spirit and born of the Virgin Mary. He suffered under Pontius Pilate, was crucified, died, and was buried. He descended to the dead. On the third day he rose again. He ascended into heaven, and is seated at the right hand of the Father. He will come again to judge the living and the dead. I believe in the Holy Spirit, the holy catholic Church, the communion of saints, the forgiveness of sins the resurrection of the body, and the life everlasting. Amen.

THE PRAYERS

All that are able to should kneel:

Minister Lord, have mercy upon us.

All **Christ, have mercy upon us.**

Minister Lord, have mercy upon us.

THE LORD'S PRAYER

All pray.

Our Father in heaven, hallowed be your Name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us. Save us from the time of trial, and deliver us from evil. For the kingdom, the power, and the glory are yours, now and for ever. Amen.

Minister Show us your mercy, O Lord;

All **And grant us your salvation.**

Minister O Lord, save the State;

All **And mercifully hear us when we call upon you.**

Minister Endue your ministers with righteousness;

All **And make you chosen people joyful.**

Minister O Lord, save your people;

All **And bless your inheritance.**

Minister Give peace in our time, O Lord.

All **May your glory be everywhere in the world .**

Minister O God, make clean our hearts within us;

All **And take not your Holy Spirit from us.**

THE COLLECT OF THE DAY

Eternal God, for your great love for all people, you sent your Son, our Savior, Jesus Christ, to take our body, and endure the death of the cross, grant that we may follow the example of his patience and humility, as well as participate in his resurrection, through Jesus Christ our Lord. **Amen.**

SALA KWA SALAMA

Baba Mungu, uliye mkuu wa salama na mupenda wa upatano, kukujua wewe ni uzima wa milele, kukutumikia wewe ni uhuru wa kweli. Utulinde sisi watumishi wako katika mashambulio yote ya adui zetu; ili sisi tukitumainia ulinzi wako, tusiogope nguvu ya adui wo wote; kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

SALA KWA NEEMA

Muhudumu na watu wanaweza kusema pamoja.

Ee Bwana, Baba yetu ya mbinguni, Mungu Mwenyezi unayeishi milele, uliyetusaidia tuione siku hii salama; utulinde leo kwa uwezo wako mkuu, tusinguke katika zambi, wala tusingie katika hatari yo yote, lakini matendo yetu yote yaongozwe nawe, ili tuyatende siku zote yaliyo ya haki mbele yako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

MAOMBI YA KANISA

Muhudumu Tuombee Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

Mwombezi huomba kwa ajili ya mahitaji ya kanisa na ya ulimwengu pasipo kuona. Muombezi anamaliza sala kwa maneno haya:

Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina.**

Maombi mengine yanaweza kusemwa.

MATANGAZO NA SADAKA

Wimbo na kupokea sadaka.

NEEMA

Watu Wote.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mutakatifu, ukae nasi sote, milele na milele. Amina.

WIMBO YA KUTOKA

THE COLLECT FOR PEACE

O God, who art the author of peace and lover of concord, in knowledge of whom standeth our eternal life, whose service is perfect freedom: Defend us, thy humble servants, in all assaults of our enemies; that we, surely trusting in thy defense, may not fear the power of any adversaries; through the might of Jesus Christ our Lord. **Amen.**

THE COLLECT FOR GRACE

The Minister and the people say this prayer together.

O Lord, our heavenly Father, almighty and everlasting God, who has safely brought us to the beginning of this day; defend us in the same with your mighty power; and grant that this day we fall into no sin, neither run into any kind of danger, but that all our doings may be ordered by your governance, to do always that is righteous in your sight; through Jesus Christ our Lord. Amen.

PRAYERS OF THE CHURCH

Minister Let us pray for the Church and the world and let us thank God for all his goodness.

The intercessor prays for the needs of the church and the world extemporaneously. The intercessor ends the prayer with these words:

And we praise your holy name for all your servants who have departed this life, who believe in you and who fear you. We ask you to give us the grace to follow their good example, to meet them in your heavenly kingdom. Grant this, O Lord, as we ask for it from Jesus Christ your Son, our Savior. **Amina.**

Other prayers may be said.

ANNOUNCEMENTS AND OFFERING

A song is sung during the offering.

THE GRACE

All Say

The grace of our Lord Jesus Christ, and the love of God, and the fellowship of the Holy Spirit, be with us all evermore. Amen.

RECESSIONAL HYMN

WAHUDUMU WA LITURUJIA

Muhubiri/Preacher - Bikole Mulanda, Swahili Minister

Kwaya/Choir - Aleluya Kwaya

Teknolojia/Sound - Bill Young

Washemasi/Greeters & Ushers - Baya Lushiawe, Mkyombwe



602 Meander Street Phone: (325) 677-2091
Abilene, Texas 79602 Email: info@heavenlyrestabilene.org
Website: heavenlyrestabilene.org Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.facebook.com/heavenlyrestabilene)

CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Luke Waters, <i>Coordinator for Youth and Young Adult Ministries</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assistant Rector for Community Life</i>	Luke Teten, <i>Verger</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Assisting Priest</i>	Lydia Hurt, <i>Interim Office Manager</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	Donna Marcy, <i>Parish Bookkeeper</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Melody Brown, <i>Website Manager</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Austin Hackel, <i>Communications Coordinator</i>
Thomas Pavlechko, <i>Organist and Director of Music</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Shelly Reed, <i>Music Assistant, Choristers</i>	Brandon Martin, <i>Assistant Sexton</i>
Laura Dickson, <i>Music Assistant, Children's Choir</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
Carol Ann Weston, <i>Director of Children & Family Ministries</i>	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>

VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Kate Haney, *Senior Warden*; Harry Hurt, *Junior Warden*; Sharon Lawler, *Secretary*; David Christianson, Michael Christie, Dru Hall, Diane Stearns, Kimberly Brumley, Jay Hardaway, Norene Mansell, John Nichols, Mary Reyes, Elizabeth Niblo Wallace, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*